




# MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA



## JARIDA LA HALI YA HEWA KILIMO

Na. 22: Msimu wa Kilimo 2020/2021


Tathmini ya Aprili 21-30, 2021 na Matazamio Kipindi cha Mei 01-10, 2021

### MUHTASARI

- Maeneo mengi nchini yamepata mvua za juu ya wastani zilizosababishwa na uwepo wa kimbunga “Jobo”.
- Wakulima na wafugaji wanashauriwa kuendelea na shughuli za kilimo na kufuata ushauri wa maafisa ugani katika maeneo yao, pia waendeleo kufuatilia utabiri wa hali ya hewa unaotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA).

### MIFUMO YA HALI YA HEWA KATIKA KIPINDI CHA APRILI 21-30, 2021

**K**atika dekad hii, migandamizo mikubwa ya hewa iliyo kaskazini mwa Ikweta iliendelea kupungua nguvu wakati ile iliyopo kusini iliimarika, hali iliyosababisha ukanda wa mvua (ITCZ) kuelekea kaskazini. Joto la bahari katika eneo la kaskazini-mashariki ya Madagaska lilikua la juu ya wastani na hivyo kuleta mchango katika uimarishaji wa kimbunga Jobo. Uwepo wa kimbunga karibu na pwani ya nchi pamoja na ukanda wa mvua (ITCZ) ulisaidia kuongeza vipindi vya mvua katika maeneo ya mwambao wa pwani. Eneo la kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola) liliendelea kuwepo na joto la bahari la wastani hadi juu kidogo ya wastani. Hali hii ilisababisha kupunguza mchango wa mifumo ya kusababisha mvua katika maeneo ya magharibi mwa nchi.



Kielelezo 1: Mwenendo wa mvua katika kipindi cha Aprili 21-30, 2021.

### TATHMINI YA HALI YA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA APRILI 21-30, 2021

### MWENENDO WA MVUA KATIKA KIPINDI CHA APRILI 21-30, 2021

**K**utokana na mifumo ya hali ya hewa ilivyokuwa, maeneo mengi yalipata mvua za juu ya wastani (zaidi ya 400%). Hata hivyo mvua za chini ya wastani (chini ya 80%) zilipatikana katika maeneo machache ya mikoa ya Ruvuma, Manyara, Singida, Tabora, Tanga, Arusha, Dodoma na Iringa kama inavyoonekana kwenye kielelezo. Hata, hivyo ongezeko la mvua na mtawanyiko vilisababishwa na uwepo wa kimbunga ‘Jobo’ katika pwani ya bahari ya Hindi.

**K**atika kipindi cha dekad hii, mazao yaliendelea vizuri kutokana na mvua za msimu. Katika maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka, mahindi yapo katika hatua ya kubeba isipokuwa katika mkoa wa Tabora, Mtwara, Rukwa, Mbeya, Dodoma na Ruvuma ambapo mahindi yapo katika hatua ya kukomaa na baadhi ya wakulima katika maeneo hayo wameendelea na uvunaji. Zao la mpunga lipo katika hatua ya kukomaa katika mikoa ya Mbeya, Rukwa, Iringa na Tabora na baadhi ya wakulima wanaendelea na shughuli za uvunaji. Licha ya mvua zilizonyesha katika dekad ya tatu, mwezi Aprili bado katika kanda ya magharibi unyeshaji hafifu na vipindi vya ukavu vya muda mrefu vimeathiri mavuno ya zao

la mpunga hususan katika mkoa wa Tabora. Kwa ujumla, hali ya mazao mashambani ni ya kuridhisha. Katika maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua, mahindi yapo katika hatua ya jani la tatu na tisa na wakulima katika mikoa ya Kagera na Mara wameendelea na palizi ya mahindi na maharagwe. Hali ya upatikanaji wa maji na malisho kwa ajili ya mifugo na wanyamapori ilikuwa ya kuridhisha katika maeneo mengi nchini.

### HALI YA MAJI KATIKA KIPINDI CHA APRILI 21-30, 2021

**K**wa ujumla hali ya maji katika mabwawa, mabonde na mtiririko wa maji kwenye mito viliendelea kuongezeka kidogo katika maeneo mengi nchini.

### MIFUMO YA HALI YA HEWA INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA MEI 01-10, 2021

**K**atika dekadi hii, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo eneo la kaskazini mwa Ikweta inatarajiwa kuendelea kupungua nguvu, wakati ile iliyopo eneo la kusini inatarajiwa kuendelea kuimarika. Hali hii inatarajiwa kusababisha ukandamvua (ITCZ) kusalia katika maeneo ya kaskazini mwa nchi. Joto la bahari la wastani hadi juu ya wastani linatarajiwa kuendelea katika eneo la kusini magharibi mwa bahari ya Hindi. Hali ambayo inatarajiwa kusababisha uwepo wa migandamizo midogo ya hewa kusini magharibi mwa bahari ya Hindi. Aidha upande wa kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola) joto la bahari linatarajiwa kuwa juu ya wastani. Hali hii haitarajiwi kuwa na mchango mkubwa katika mifumo ya hali ya hewa inayosukuma upepo wenye unyevunyevu kutoka misitu ya Congo kuelekea katika maeneo ya magharibi mwa nchi.

### HALI YA HEWA INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA MEI 01-10, 2021

**M**aeneo ya kanda ya Ziwa Viktoria (mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara), mikoa ya magharibi mwa nchi (Kigoma, Katavi na Tabora), pwani ya kaskazini (mikoa ya Tanga, maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba) na nyanda za juu kaskazini mashariki (mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro) yanatarajiwa kuwa na vipindi vya mvua zitakazoambatana na ngurumo katika baadhi ya maeneo.

Pwani ya kusini (mikoa ya Mtwara na Lindi) kanda ya kati (Dodoma na Singida), nyanda za juu kusini magharibi (mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa) na kanda ya kusini (mkoa wa Ruvuma na maeneo ya kusini mwa Morogoro) yanatarajiwa kuwa na mvua nyepesi katika maeneo machache.

### HALI YA HEWA KILIMO: MATARAJIO NA USHAURI KIPINDI CHA MEI 01-10, 2021

**M**vua zinazotarajiwa zitaendelea kuimarisha unyevunyevu kwenye udongo kwa ajili ya mazao na malisho hususan kwa maeneo yanayopata mvua za masika. Hata hivyo mvua chache na nyepesi zinazotarajiwa katika maeneo yanayopata mvua za msimu hususan katika mikoa ya Mbeya, Iringa, Rukwa, Mtwara, Lindi, Dodoma, Singida na Ruvuma zitasaidia katika shughuli za uvunaji wa mazao yaliyokauka. Wakulima katika maeneo hayo wanashauriwa kuandaa maghala au sehemu maalum kwa ajili ya kuhifadhi mazao yao. Pia wakulima katika maeneo yanayopata mvua za masika wanashauriwa kufuata ushauri wa maafisa ugani na kuchukua hatua stahiki katika kutunza mashamba na matumizi ya pembejeo kama vile mbolea na viuatilifu. Wafugaji na wavuvi wanashauriwa kupata ushauri wa maafisa ugani husika ili kudhibiti magonjwa ya mifugo na athari nyingine zitokanazo na hali ya hewa inayotarajiwa. Pia, wakulima wanashauriwa kuendelea kufuatilia utabiri wa hali ya hewa.

### HALI YA MAJI INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA MEI 01-10, 2021

**K**ina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito vinatarajiwa kuongezeka kidogo katika maeneo mengi hususan yanayopata mvua za masika. Hata hivyo watumiaji rasilimali maji wanashauriwa kuvuna maji ya mvua kwa ajili ya matumizi ya baadae.